MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21 KUJITAYARISHA KWA SARAFI YAKO

*Bofya aikoni hizi kote kwa maelezo husika unayoweza kuhitaji safari yako.*

*Kiungo kinakuja hivi karibuni*

1

## Gredi za PK-5

Si mapema sana kuwazia matarajio na ndoto ulizo nazo juu ya mtoto wako; tazama mpango wa safari wa utotoni kwa taarifa zaidi.

2

## Gredi za 6 hadi 8

Wilaya za shule zinahitajika kuunda mpango wa ufanisi kwa wanafunzi walio katika hatari ya kuacha shule, kwa kuzingatia sera ya shule ya ushauri wa taaluma.

3

## Kufikia Umri wa Miaka 14

Wilaya za shule zinatakiwa kuunda Mpango wa Mpito katika IEP ambao huanza kutumika mwanafunzi anapofika umri wa miaka 14 au chini ikiwa inafaa. Wakazi wa Ohio wenye ulemavu wanastahiki kutuma maombi ya kupata huduma za urekebishaji wa ufundi kwenye shirika la Opportunities for Ohioans with Disabilities

4

## Gredi ya 9

Wilaya za shule zinahitajika:

- kuunda na kuendeleza mpango wa kuhitimu kwa wanafunzi wote wanaoingia gredi ya 9 hadi ya 12
- kumjulisha mzazi kila mwaka ikiwa mwanafunzi anatambuliwa kuwa katika hatari ya kutofuzu kupata diploma ya shule ya upili

## Sehemu ya 1 ya Huduma

## Sehemu ya 2 ya Huduma

5

## Umri wa Miaka 16

Ikiwa mtoto wako anapokea huduma za ulemavu katika ukuaji za bodi ya kaunti, ustahiki hukaguliwa kwa wakati huu.

6

## Umri wa Miaka 17

Wilaya ya shule lazima ikujulishe wewe pamoja na mtoto wako kuhusu uhamishaji wa haki kwa mtoto afikapo umri wa miaka 18

7

## Umri wa Miaka 18

Mwanafunzi ana haki na wajibu wa kufanya uchaguzi fulani wa kisheria na kielimu ambao wazazi wamemfanyia hapo awali, kama vile kuidhinisha IEP yake.

## Mtoto wako amemaliza shule ya upili

Wilaya za shule zinatakiwa kutoa muhtasari wa utendaji

8

## Umri wa Miaka 22

Watu hawastahiki tena elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) chini ya Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (IDEA) ya Ohio.

Ohio | Department of Education

MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21

## KUJITAYARISHA KWA SARAFI YAKO

### KUWEKA VITU UTAKAVYOHITAJI KWENYE MKOBA

Kama ilivyo kwa safari yoyote ile, kupanga kunaweza kukusaidia kufanya zaidi ya kile unachotaka na kukusaidia kufurahia safari. “Mkoba wa Mpito” una tovuti, nyenzo na zana nyingi za kukusaidia wewe na mtoto wako kujiandaa kwa maisha ya baada ya shule ya upili. Unapojitayarisha kwa safari yako ya mpito, tumia mkoba wako na Mpango wa Safari ya Mpito ili kukusaidia kukuongoza. Kwa kufuata Mpango huu wa Safari ya Mpito, unapaswa kuwa tayari kwa ajili ya kuondoka kwa mtoto wako shuleni na kuendelea na maisha ya baada ya shule ya upili.

- Zana ya Kukuongoza kuhusu Mashirika - Zana ya Kukuongoza kuhusu Mashirika ni nyenzo ya kutoa taarifa za msingi na kuhusu mashirika muhimu ambayo yanaweza kuhusika wakati wa mpito wa kijana kuwa mtu mzima. Zana hii ni muhimu kwa vijana, familia zao, shule na mashirika.
- Mwongozo wa Wazazi wa Mfumo wa Kusaidiwa Kupata Kazi - Mwongozo wa Wazazi wa Mfumo wa Kusaidiwa Kupata Kazi ni mwongozo wa kusaidia familia kushawishi na kujenga uhusiano wa kutafutiana kazi wakiwa nyumbani.
- Kupanga Mwelekeo wa Maisha - Mwongozo wa Kupanga Mwelekeo wa Maisha ni kundi la zana zinazotumiwa na watu binafsi wenye ulemavu na familia zao ili kupanga mawazo, maono na malengo, pamoja na kutatua matatizo, kutafuta na kupata usaidizi.
- Manufaa ya Msingi ya Walemavu - Manufaa ya Msingi ya Walemavu hukupa zana na taarifa kuhusu ajira, bima za afya na manufaa. Watu wanaweza kujifunza jinsi kazi na manufaa huenda pamoja.
- Upangaji wa Mpito wa Mapema - Kadri familia na washirika wanavyoanza kuwaza mapema kuhusu maisha ya mtu mzima, ndivyo vijana watakavyoweza kujitayarisha zaidi kwa maisha yao ya baadaye. Angalia tovuti hii kwa nyenzo, usaidizi na shughuli ambazo zitawashirikisha wanafunzi wadogo ili kuwasaidia kuanza kuwaza jinsi maisha ya mtu mzima yenye kuridhisha yanaweza kuwa.
- Washauri wa Wazazi - Washauri wa Wazazi wa Ohio wanapatikana ili kusaidia familia kuelewa taratibu na huduma maalum za elimu kwa mtoto wao. Katika tovuti ya Ohio Parent Mentor Project kutoka Chuo Kikuu cha Ohio State na Ohio Department of Education, utapata maeneo ya washauri wa wazazi wa Ohio, video na zana za kusaidia katika kutumia utaratibu wa elimu maalum, na nyenzo za kujifunzia nyumbani.
- Muungano wa Ohio wa Elimu ya Watoto wenye Ulemavu - Muungano wa Ohio wa Elimu ya Watoto wenye Ulemavu (OCECD) ni shirika lisilo la faida la jimbo lote linalohudumia familia za watoto wachanga, watoto wanaoanza kutembea, watoto na vijana wenye ulemavu katika Ohio, walimu na mashirika ambayo hutoa huduma kwao.
- Timu za Usaidizi wa Jimbo za Idara ya Elimu ya Ohio - Kama sehemu ya Mfumo wa Usaidizi wa Jimbo Lote, Timu ya Usaidizi ya Jimbo hushirikiana na shule, familia, washirika wa kieneo na Idara kupitia mchakato endelevu wa uboreshaji ili kuhakikisha kila mtoto katika Ohio anapata elimu ya ubora wa juu.
- Inuka (Rise Up) - Inuka ni mwongozo uliotayarishwa na shirika la Disability Rights Ohio (DRO) kwa vijana wenye umri wa mpito kuanzia umri wa miaka 14 hadi 21. Mwongozo huu una taarifa muhimu kuhusu hali ambazo watu wanaweza kupitia wanapokuwa watu wazima.
- Akaunti ya STABLE - Akaunti ya STABLE ni akaunti ya uwekezaji inayopatikana kwa watu wanaostahiki wenye ulemavu. Akaunti za STABLE hukuwezesha kuhifadhi na kuwekeza pesa bila kupoteza ustahiki wa mipango fulani ya misaada ya serikali, kama vile Medicaid au Supplemental Security Income (SSI). Mapato katika akaunti yako ya STABLE hayatatozwa kodi ya mapato ya serikali ya shirikisho, mradi tu uyatumie kwa gharama zinazostahiki za walemavu.
- Kituo cha Ushirikishaji wa Familia cha Jimbo Lote - Kituo cha Ushirikishaji wa Familia cha Jimbo Lote la Ohio huwawezesha wanafunzi, wazazi, walezi, viongozi wa shule na washirika wa jamii kuunda mahusiano bora na shirikishi baina yao ili kuunga mkono mafanikio ya kielimu ya wanafunzi wa gredi za K-12.

RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI

MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21

## Mtoto wako katika gredi za PK-5

Si mapema sana kuanza kufikiria na kuzungumzia kuhusu matarajio yako juu ya maisha ya mtoto wako.

- Usaidizi wa Mapema, unaojulikana kama EI, ni mfumo wa jimbo lote unaotoa huduma zilizoratibiwa kwa wazazi wa watoto wanaostahiki walio chini ya umri wa miaka 3 walio na ucheleweshaji wa ukuaji au ulemavu. EI ni sehemu ya mfumo wa usaidizi wa Help Me Grow. Huduma na usaidizi huu unaotolewa kwa watu wenye ulemavu wa ukuaji hutolewa katika ngazi ya kaunti na bodi ya eneo lako ya ulemavu wa ukuaji (CBDD). CBDD huamua ustahiki, hutathmini mahitaji yako, na huratibu ni huduma zipi zinaweza kukusaidia vyema zaidi. Bofya kiungo hiki kwa taarifa kuhusu ustahiki wa huduma ya usaidizi wa mapema.
- Idara ya Elimu ya Ohio pia inaunda mpango wa safari wa utotoni ili kukusaidia katika elimu ya mtoto wako katika umri huu mdogo. Rejelea tovuti ya Idara katika miezi michache ijayo ili kutazama nyenzo hii mpya.
- Idara ya Elimu ya Ohio ina zana zinazozisaidia familia na shule katika upangaji wa usaidizi wa mapema. Kwa mfano, zana kama vile Kupanga Mwelekeo wa Maish inaweza kuzisaidia familia kuanza kuzungumzia kuhusu mpito.

## Mtoto wako katika gredi za 6-8

- Mpango wa Mafanikio ya Mwanafunzi ni mchakato unaolenga wanafunzi wa kuwasaidia pamoja na familia zao kuelewa mahitaji ya kimasomo ili kufikia lengo la kitaaluma. Ikiwa mtoto wako yuko katika hatari ya kuacha shule, wilaya ya shule ya mtoto wako inahitajika kuunda Mpango wa Mafanikio ya Mwanafunzi kwa ajili yake.
- Kabla ya wilaya ya shule kuunda Mpango wa Mafanikio ya Mwanafunzi, lazima ikualike kwenye mkutano ili usaidie katika kuunda mpango. Wilaya ya shule lazima pia ishiriki nawe Mpango wa Mafanikio wa Mwanafunzi wa mtoto wako baada ya kuundwa.

RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI

MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21

## Mtoto wako anafikisha umri wa miaka 14

- Wilaya ya shule ya mtoto wako lazima iunde mpango wa mpito kwa mtoto wako, Sehemu ya 5 ya Mpango Mahususi wa Elimu (IEP, Mpango Mahususi wa Elimu).
- Wilaya ya shule ya mtoto wako itakusanya taarifa kuhusu mtoto wako kupitia tathmini za mpito zinazolingana na umri (AATA). Taarifa hizi zinajumuisha mapendeleo, shauku, mahitaji na uwezo wa mtoto wako – taarifa hizi wakati mwingine hujulikana kama PINS.
- Wilaya ya shule ya mtoto wako lazima itumie taarifa zilizokusanywa kupitia mchakato wa AATA kuunda mpango wa mpito. Mpango wa mpito wa mtoto wako utajumuisha taarifa kuhusu yafuatayo:
  - huduma za mpito,
  - kozi za masomo,
  - malengo ya baada ya shule ya upili kuhusiana na mafunzo na elimu
  - malengo ya baada ya shule ya upili kuhusiana na ujuzi wa maisha ya kujitegemea (ikiwa inafaa), na
  - malengo ya baada ya shule ya upili kuhusiana na ajira yenye ushindani na jumuishi.

## Mtoto wako anaingia gredi ya 9

- Kuanzia gredi ya 9 na kuendelea hadi kuhitimu, shule ya mtoto wako inahitajika kushirikiana na mtoto wako (na kukualika katika mchakato huu) ili kuunda mpango wa kuhitimu shule ya upili.
- Kuna masharti mengi kwa wanafunzi ili wahitimu shule ya upili. Mpango wa kuhitimu unapaswa kupanga kile mtoto wako anahitaji kufanya ili kukidhi masharti hayo. Mpango unaposasishwa kila mwaka, unapaswa kurekodi mafanikio (au mapungufu) ya mtoto wako katika kutimiza masharti ya kuhitimu. Iwapo mtoto wako atakuwa katika hatari ya kutohitimu kwa sababu hajatimiza masharti moja au zaidi, wilaya ya shule lazima ikujulishe.

RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI

MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21

## SEHEMU YA 1 YA HUDUMA

Sehemu ya kwanza ya huduma ina maelezo ambayo huishia kuwa muhimu zaidi kwa mtoto wako afikapo umri wa miaka 14. Kiungo cha kwanza kitakupeleka kwenye mwongozo wa kupanga Tathmini ya Mpito Inayolingana na Umri (unaweza kusikia ukirejelewa kama AATA). Tathmini ya mpito inayolingana na umri ni muhimu ili kumsaidia mtoto wako kupata elimu, mafunzo na usaidizi anaohitaji ili kukuza maarifa na ujuzi utakaomsaidia kufikia malengo yake ya maishani. Kiungo cha pili, Orodha Hakikishi ya Kiashirio cha 13, hutoa maswali yanayoweza kukuongoza wewe na timu ya mpango wa elimu binafsi wa mtoto wako (IEP) katika kubainisha kama kuna malengo yafaayo ya baada ya shule ya upili katika nyanja za mafunzo, elimu, ajira, na ujuzi wa maisha ya kujitegemea. Zana hizi zinaweza kukuwezesha kumsaidia mtoto wako anapojiandaa kwa maisha baada ya shule ya upili.

- Mwongozo wa Upangaji wa Tathmini ya Mpito Inayolingana na Umri
- Orodha Kaguzi ya Kiashiria cha 13 - *(Kiungo kitawekwa hivi karibuni)*

## Mtoto wako anafikisha umri wa miaka 16

- Mtoto wako anapofikisha umri wa miaka 16, ikiwa mtoto wako amestahiki huduma chini ya bodi ya kaunti ya ulemavu wa ukuaji, ustahiki wake hautegemei tena Zana ya Kuamua Ustahiki wa Watoto wa Ohio (Children's Ohio Eligibility Determination Instrument (COEDI)). Ustahiki wake sasa utabainishwa kupitia Zana ya Kuamua Ustahiki ya Ohio (Ohio Eligibility Determination Instrument (OEDI)). Ikiwa mtoto wako anapokea huduma hizi na unatarajia kuziendeleza, basi Mwongozo wa Mtumiaji wa OEDI unaweza kukusaidia katika mchakato huu.

**RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI**

## SEHEMU YA 2 YA HUDUMA

Sehemu ya pili ya huduma ina viungo viwili vinavyotoa taarifa kuhusu jinsi ya kupata leseni ya udereva na kitambulisho cha Ohio. Kadi za vitambulisho vya picha ni za utambulisho pekee na zinaweza kusaidia kumpata mtoto wako, ikiwa atapotea. Hakuna umri wa chini wa kuomba kadi ya kitambulisho cha Ohio. Anaweza kupata kibali cha muda cha udereva akifikia umri wa miaka 15 unusu na anaweza kupata leseni ya udereva ya majaribio miezi sita baada ya kuwa na kibali cha udereva.

- Kitambulisho cha Jimbo
- Leseni ya Udereva

## Mtoto wako anafikisha umri wa miaka 17

- Umri wa uwajibikaji mwingi ni umri ambao mtu huchukuliwa kuwa mtu mzima. Umri wa uwajibikaji mwingi katika Ohio ni miaka 18.
- Angalau mwaka mmoja kabla ya mtoto wako kufikisha umri wa uwajibikaji mwingi, wilaya ya shule lazima ikujulishe wewe na mtoto wako kwamba haki za IDEA zitahamishiwa kwa mtoto wako afikapo umri wa miaka 18. IEP ya mtoto wako lazima ionyeshe kwamba wewe na mtoto wako mmefahamishwa kuhusu haki zake. Wilaya yako ya shule inawajibu kwa nyote kuendelea kumsaidia mtoto wako katika umri wa miaka 18 ikiwa inahitajika.

RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI

MPANGO WA SAFARI YA

# Mpito wa shule ya upili

KWA FAMILIA ZILIZO NA WATOTO WALIO NA ULEMAVU, WENYE UMRI WA MIAKA 3 HADI 21

## Mtoto wako anafikisha umri wa miaka 18

- Mtoto wako ana haki na wajibu wa kujifanyia maamuzi fulani ya kisheria na kielimu.

## Mtoto wako amefika mwisho wa shule ya upili

Mtoto wako yuko tayari kuanza safari ya mtu mzima. Mkoba wake umejaa nyenzo za kumsaidia katika safari yake.

- Mtoto wako anapohitimu au kuondoka shule ya upili, wilaya ya shule ya mtoto wako lazima itoe muhtasari wa utendaji wa kimasomo na kiutendakazi wa mtoto wako. Muhtasari huu unapaswa pia kujumuisha mapendekezo yanayoweza kumsaidia mtoto wako kufikia malengo yake ya baada ya shule ya upili.
- Unaweza kuchangia mafanikio ya mtoto wako baada ya shule ya upili kwa kumsaidia kufanya maendeleo ya kutimiza mapendekezo anayopewa.

## Mtoto wako anafikisha umri wa miaka 22

- Mtoto wako hastahiki tena kupata elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) chini ya Individuals with Disabilities Education Act (IDEA, Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu). Ikiwa mtoto wako atafikisha umri wa miaka 22 wakati wa mwaka wa shule, sera ya wilaya ya shule itabaini kama mtoto wako anaweza kumaliza mwaka wa shule kwenye wilaya.

RUDI KWENYE MPANGO WA SAFARI